JINA…….... NAMBARI.....

SHULE:.....…….....

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Tangu zama kongwe za mawe maisha ya binadamu yamepitia katika awamu mbalimblali za kimaendeleo; yawe ya kisayansi, kiuchumi, kijamii au hata kisiasa. Katika kipindi chote ambacho binadamu ameishi katika ulimwengu huu, utamaduni umekuwa sehemu muhimu ya maisha yake. Utamaduni huu unaweza kuangaliwa kwa namna mbalimblai. Upo utamaduni finyu, ambao unahusisha jamii moja dogo mathalan, katika, ukoo au eneo dogo.

Kwa upande mwingine kuna utamaduni pana ambao unaihusisha jamii nzima. Mathalan, nchi Fulani inaweza kuwa na matendo, imani, thamani na fikira ambazo ni msingi mkubwa katika nchi hiyo. Hizi huwa msingi wa utamaduni wa kitaifa. Utamaduni huu ndio ambao unamtenga raia wa nchi moja na raia wa nchi nyingine. Utamaduni wa kitaifa ni nguzo muhimu ya uzalendo wa wanataifa maalum; unawatambulisha na wanaouonea fahari. Vipengele vya utamaduni wa kitaifa hutokeza kwa njia mbalimbali kama mavazi, vyakula, lugha, itikadi au hata mtazamo wa raia wa nchi mahsusi. Tumbi kubwa ya nchi za ulimwengu huwa na utamaduni unaozitambulisha na ambao humfanya raia ajinabi kuweza kuwatambua raia hao. Utamaduni ni kitovu cha uhai wa jamii yote ile. Licha ya ukweli huu, ni muhimu, inahalisi kutambua kuwa maisha ya binadamu huathiriwa na kani mbalimbali zinazotokea katika mazingira yake ya kila siku. Kani hizi huweza kuwa vyanzo vya mabadiliko ya sifa fulani zinazohusishwa na utamaduni wake. Maendeleo ya kiwakati ambayo huenda sambamba na mahitaji anuwai ya kimaisha huweza kuwa chanzo cha kuachwa kwa tamaduni fulani. Hata hivyo, binadamu sio sifongo ambalo huftyonza maji yote, maji machafu na maji safi pasi na kubagua. Binadamu mwenye akili razini anapaswa kuchuja na kutathmini ni amali au thamani zipi mpya ambazo anaweza kuzichukua na labda kuupuza baadhi ya thamani za kale zisizomfaa. Kigezo kikuu kinachomsadia ni kitambua mahitaji yake sambamba na wakati anamoishi. Mathalan, katika maisha ya zamani, uchumaji ulitegemea ubabe kwa kiasi kikubwa lakini siku hizi ubabe sio kigezo cha uchumaji kwa kiasi kikubwa.

Akili ni msingi mkubwa sana siku hizi katika uchumaji au kutarazaki. Inahalisi basi kuuza sifa za kitamaduni ambazo zinaelekea kuutilia mkazo mkubwa kwenye matumizi ya nguvu au ubabe. Yapo matendo mengi katika jamii ambayo yalidhibitiwa na imani za kishirikina kabla

ya nuru ya elimu kulimulika giza la ujinga lililotamalaki katika jamii. Ikiwa jamii itaendelea kuyatenda matendo haya basi ile itakuwa ni jamii ambayo ni kama imezunguka palepale. Ile itakuwa ni jamii ambayo imeshindwa kuendelea.

MASWALI

(a) Ipe kichwa taarifa hii. (Alama 1)

…….....……

(b) Taja aina mbili za tamaduni. (Alama 2)

…….....…

(c) Taja mifano minne ya vigezo vya utamaduni wa kitaifa. (Alama 4)

……

(d) Eleza umuhimu wa taifa kuwa na utamaduni wake. (Alama 4)

(e) " Tembea na majira". Fafanua usemi huu kwa kutumia maelezo ya taarifa. (Alama 2)

(f) Eleza maana ya (Alama 2)

(i) Raia ajinabi

……

(ii) lililotamalaki katika jamii

……

…….....……

2. MUHTASARI

Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali.

Nchi nyingi duniani zimetia saini mkataba wa Umoja wa Maataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saini, nchi hizi zimetangaza kujitolea kwao kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake na kuwa watoto wote katika hilaya zao wananufaika kutokana na haki hizi.

Miogoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye viinilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha, kila mtoto ana haki ya kutopigwa na kutodunishwa kwa namna yoyote, iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo. Mtoto ana haki pia kutolazimishwa kufanya kazi za kiutumwa, nzito na za kushurutishwa. Halikadhalika, ana haki ya kuishi katika nyumba au makazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauka ya haya, ana haki ya kupata

huduma za afya, mahitaji maalumu, michezo, upendo na habari. Isitoshe, anastahili kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Haki hizi zinatakiwa

kulindwa na kila mwanajamii, hivyo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. La kusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilinda haki hizi ndio wanoongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje. Wengine hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifu yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wangeuza kuwa mibaba ya kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasioenda shule kwa sababu ya lindi la ufukara uliokithiri. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo. Wanaong'ang'ana iwepo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana. Jiulize, watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba ' vishilingi"?

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma,mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

Maswali

(a) Fupisha aya mbili za kwanza (maneno 65-70) (Alama 8)

Nakala chafu

……

……

……

Nakala Safi

(b) **Eleza** ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa.(Maneno 30-35) (Alama 4)

Nakala chafu

……

……

……....

.....……

Nakala safi

……

……

……

3. **Matumizi ya lugha**

(a) Sauti / p / ni kipasuo. Sauti hizi ni gani? (Alama 2)

(i) / f /

……

(ii) / l /

……

(b) Eleza maana ya maneno haya kulingana na shadda (mkazo). (Alama 2)

(i) bara'bara

……

(ii) ba'rabara

……

(c) Nyambua vitenzi vifuatavyo vya silabi moja ili kujaza mapengo (Alama 2)

(i) Mgeni ali ……. (pa, kutendewa) kiti ili akae.

(ii) Ame ..... (la, kutendesha) mtoto chakula

(d) Toa maana mbili ya sentensi hii (Alama 2)

(i) Nionyeshe vile nitakavyobeba.

……

……

..……

(e) Badilisha kwa msemo halisi (Alama 3)

Rais alisema kuwa angesafiri kwenda Dubai siku hiyo alasiri.

……

……

(f) Kwa kutolea mifano ya sentensi, bainisha matumizi matatu ya ritifaa (kibainishi) (Alama 3)

(i) ……

(ii) ……..

(iii) …….

(g) Tumia viunganishi hivi mwanzoni mwa sentensi kuonyesha matumizi yake (Alama 2)

(i) Ikiwa

……

(ii) Labda

……

(h) Ainisha mofimu katika sentensi hii (Alama 3)

Aliyemletea.

……

(i) Onyesha kirai kivumishi na kirai kielezi katika sentensi hii. (Alama 2)

Vitabu vyote vimeibwa leo asubuhi

……

(j) Kwa kutunga sentensi, tofautisha vitate hivi (Alama 2)

(i) Baka

……

(ii) Paka

……

…….....……

(k) Chagua kihisishi mwafaka kati ya hivi kujazia mapengo. (Alhamdulilahi! Salaale! Ebo!)

(Alama 3)

(i) _____mtu hawezi kuingiza kidole kinywani mwa simba.

(ii) _____ aliweza kuruka juu kiasi hicho.

(iii) _____ amekamatwa, Mungu halali, ameibia watu wengi sana.

(l) Kamilisha jedwali (Alama 3)

Kitenzi	kivumishi
Potea	
	Karimu
Dhuluma	

(m) Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia mistari (vishale) (Alama 4)

Baba na mama wataenda sokoni.

……

……

(n) Geuza sentensi ifuatayo katika ukubwa. (Alama 2)

Mtoto alitishwa na mtu mrefu ajabu.

……

(o) Andika upya sentensi hii ukifuata maagizo. (Alama 2)

Kalamu ilipopotea, mwalimu alikasirika.

Anza:Kupotea ……...

…….....

(p) Onyesha kitondo, kipozi na chagizo katika sentensi hii (Alama 3)

Mwanafunzi alifanyiwa mtihani jioni.

……

…….....

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua sifa za lugha ya sehemu za kuabudu. (Alama 10)